JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

MAMLAKA YA UDHIBITI WA
NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO

CEREALS AND OTHER PRODUCE REGULATORY AUTHORITY

## TAARIFA KWA UMMA

## KUFUNGULIWA KWA MSIMU WA MAUZO YA ZAO LA UFUTA

**24 APRILI 2025**

Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) inawatangazia wananchi wote (Wakulima, Wanunuzi na Wadau wengine) katika Mikoa yote inayozalisha zao la ufuta Tanzania Bara kuwa msimu wa mauzo ya zao la ufuta utafunguliwa rasmi tarehe 25 Aprili, 2025. Katika msimu huu wa mauzo, zao la ufuta litauzwa kwa kutumia mfumo wa stakabadhi za ghala kupitia minada ya kidijitali katika mikoa yote inayozalisha zao hilo ikiwemo Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa, Rukwa, Katavi, Kigoma, Tabora, Dodoma, Singida, Manyara, Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro na Pwani.

Wafanyabiashara wote wa ufuta wanakumbushwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kupitia tangazo la **tarehe 09 Januari, 2025 lililohusu Orodha ya Mazao ya Mikunde na Mbegu za mafuta (Choroko, Ufuta, Dengu, Mbaazi na Soya) yatakayouzwa kwa mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Minada ya Kidijitali msimu wa 2024/2025**. Kupitia tangazo hilo, wafanyabiashara wa mazao hayo hawaruhusiwi kununua mazao tajwa nje ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Ratiba ya minada katika maeneo mbalimbali ya mikoa tajwa itatolewa na COPRA ambapo mnada wa kwanza unatarajiwa kufanyika katika mkoa wa **Songwe, tarehe 3 Mei, 2025**.

Wafanyabiashara wote wanaojihusisha na ununuzi wa mazao nje ya mfumo rasmi, au kusafirisha mazao nje ya nchi bila vibali halali, au kwa kutumia vibali vya kughushi, wanatekeleza vitendo vinavyokiuka sheria. Kutokana na ukiukwaji huo, Mamlaka itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya wahusika, zikiwemo: **kutaifisha mazao yaliyonunuliwa au kusafirishwa kinyume na utaratibu**, **kuwazuia kushiriki katika shughuli za ununuzi wa mazao ndani ya nchi**, **kutozwa faini**, pamoja na **kufikishwa Mahakamani kwa mujibu wa Kifungu cha 22 cha Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249**.

Imetolewa na,

**MKURUGENZI MKUU**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO**

*Jengo la Kahawa Plaza, Mtaa wa Njedengwa, S.L.P 2780, Dodoma -Tanzania.*

*Simu: 0800 11 77 77, Barua pepe: info@copra.go.tz.*